







**STARLINK** | ADAPTA YA BOMBA YA PERFORMANCE



**Kilicho ndani ya Kasha**

Kiunzi cha Adapta ya Bomba

Skurubu za M6 za Kichwa  
cha Kifungo (4)Ufunguo wa Pembe  
Sita (2)Milimita 99  
(inchi 3.9)Milimita 252  
(inchi 9.9)Milimita 233  
(inchi 9.2)Milimita 218  
(inchi 8.6)Milimita 38-60  
(inchi 1.5 - 2.4)

## 1 | Pakua Programu ya Starlink


Changanua msimbo wa QR ili upakue Programu ya Starlink.



## 2 | Chomeka Kebo ya Starlink


Fungamanisha ncha ya kiunganishi cha Performance ya kebo ya Starlink iliyoonyeshwa kwa mkato mwekundu na uichomeke kwenye Starlink yako kwa kushikilia ncha ya plagi na kuingiza kabisa kwenye sahani.

Ikiwa kebo ya Starlink inahitaji kuondolewa, zungusha kola kinyumenyume kisha uvute ili uitenganishe na Starlink yako.




### 3 | Funga Adapta ya Bomba Kwenye Starlink

Funga skurubu za mashine ulizopewa kupitia adapta ya bomba ziingie kwenye sehemu ya nyuma ya Starlink na ukaze skurubu nne ukitumia ufunguo wa pembe sita. Kaza skurubu kwenye kona zote 4 hadi bolti zifiki N·m 7 (lb·ft 5.2). Hakikisha kiunzi kimeunganishwa imara kwenye Starlink.



### 4 | Legeza Skurubu za Kushikiza


Kwa kutumia ufunguo wa pembe sita, legeza skurubu za kushikiza kwenye Adapta ya Bomba hadi tundu liwe kubwa nya kutosha kutoshea bomba lako la kufunga.



## 5 | Funga Starlink kwenye Bomba

Ingiza Adapta ya Bomba kwenye bomba lako la kufunga. Kaza skurubu za kushikiza kwa muda ili kuhakikisha Starlink inakaa thabiti kwenye bomba.


Unganisha ncha ya pili ya kebo ya Starlink kwenye kigawi cha umeme na uchomeke kwenye soketi ya umeme.





## 6 | Fungamanisha Starlink Yako

Arifa kwenye Programu itaonyesha ikiwa unahitaji kuzungusha Starlink ili ifungamanishwe vizuri.

Bofya arifa ili kutumia zana ya kufungamanisha.





## 7 | Funga Mfungamanisho

Kwa kutumia ufunguo wa pembe sita, kaza skurubu za kushikiza kwenye Adapta ya Bomba ili kufunga Starlink yako mahali pake.

Hakikisha Starlink yako imeunganishwa kwa uthabiti.

